**HOTUBA YA MHESHIMIWA MAMA SALMA KIKWETE KATIKA UZINDUZI WA UMOJA WA VIKUNDI VYA WAMA WILAYA YA KINONDONI ( UWAMAKI) TAREHE 18 DISEMBA, 2014**

***Mheshimiwa Said Meck Sadik Mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam,***

***Mheshimiwa Jordan Rugimbana Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni ,***

***Mheshimiwa Idd Azan Mbunge wa Jimbo la Kinondoni,***

***Mheshimiwa Mwenda Meya wa Manispaa ya Kinondoni ,***

***Mwenyekiti wa UWAMAKI,***

***Waheshimiwa Madiwani,***

***Waheshimiwa Wabunge mliohudhuria,***

***Viongozi wa Chama na Serikali Mliohudhuria,***

***Waandishi wa habari ,***

***Wanavikundi,***

***Wageni Waalikwa,***

***Mabibi na Mabwana,***

**Habari ya Asubuhi.**

Napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kujumuika pamoja siku ya leo. Aidha nitumie fursa hii kuwapongeza wale wote walioshiriki katika kufanikisha shughuli hii hususan viongozi na wanavikundi wa UWAMAKI. Kutokana na kazi nzuri mliyoifanya na mnayoendelea kuifanya ndio maana leo hii tunasherehekea matunda ya kazi hiyo ambayo ni mchango mkubwa kwa maendeleo na jamii kwa ujumla.

Sitakuwa nimewatendea haki iwapo sitawashukuru wadau na Taasisi mbalimbali kwa kushirishirikiana na wanavikundi hawa katika kufanikisha malengo yao. Lakini pia niwashukuru, viongozi wa serikali katika idara mbalimbali kwa kuwawekea wanavikundi mazingira mazuri ya kufikia malengo yao.

*Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana,*

Sherehe hii ya kuzindua **Umoja wa Vikundi vya WAMA Wilaya ya Kinondoni, ( UWAMAKI)** ni muendelezo wa kazi ya Taasisi ya WAMA ya kuanzisha vikundi na kuunda Umoja wa vikundi, kwa lengo la kutengeneza muundo wa kuratibu na kuhudumia vikundi katika kila Kata na Wilaya nchini. Mpaka sasa kwa Mkoa wa Dar es Salaam tumeshaunda Umoja Kata ya Majohe kwa ajili ya Wilaya ya Ilala, na Mbagala kwa ajili ya Wilaya ya Temeke. Katika maeneo hayo, Taasisi ya WAMA inahudumia wanavikundi walio chini ya Umoja wasiopungua 725.

Vikundi hivi vimepata fursa ya kupata mafunzo ya Kuweka na Kukopa, na fursa za mafunzo ya kupata ujuzi na kujiunga katika mitandao mbali mbali ya kiuchumi.

Kama ambavyo mmeweza kusikia katika risala ya wanavikundi jumla ya shilingi **79,739, 000/=** zimekusanywa na kati ya hizo shilingi **47,500, 000/=** zimekopeshwa kwa wanavikundi wa wilaya ya Kinondoni. Mradi huu wa kuwawezesha wanawake kwa kuwapa mafunzo kupitia vikundi, unafanyika pia katika Mkoa wa Lindi, Pwani na Dar es Salaam. Ambapo hadi kufikia mwezi wa Septemba mwaka huu 2014 jumla ya watu 18,000 wamefikiwa kwa kupitia vikundi 688 vilivyoundwa, na tayari jumla ya shilingi milioni 277 zimekusanywa na kukopeshwa.

***Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana,***

Mafanikio haya ambayo tunayasikia leo ni jitihada zilizofanywa na wanawake wenyewe kwa kupata usimamizi na muongozo.

Napenda kutoa wito kwa wadau wote kuunga mkono jitihada zao kwa kuwaunganisha na huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Pia nitumie fursa hii kuwaasa wanavikundi; Mafanikio mliyopata yasiwaridhishe bali muendelee kutafuta njia mbalimbali za kupiga hatua hususan katika kupata utaalamu wa kuboresha bidhaa zenu, kutafuta masoko zaidi na kufanya ubunifu wa kuweza kuvumbua bidhaa na biashara nyingine tofauti ili kuondokana na ushindani kati yenu. Kwani mnapokuwa na bidhaa zinazofanana itawaweka katika mazingira ya kushindania soko jambo ambalo litapunguza kiasi cha mauzo ambayo ndio pato lenu wajasiriamali. Jitihada ifanywe katika kutafuta wataalam ambao watawapa mafunzo ya kukuza biashara, ambapo mara kadhaa Taasisi ya WAMA imekuwa ikitoa mafunzo hayo kwa kushirikiana na shirika la kazi Duniani ILO.

Wakati sasa umefika wa kuwashirikisha vijana wa kike na wa kiume katika shughuli hizi za vikundi ili walete mawazo mapya na ubunifu, na wakati huo ni kutoa fursa kwa vijana katika kujitengenezea mazingira ya kujiajiri. Kwani vijana wengi wana elimu na ujuzi ambao wameupata masomoni lakini wanakabiliwa na tatizo la kukosa ajira. Kupitia vikundi hivi vijana wanaweza kupata mitaji yao midogo  midogo pamoja na mafunzo ya kuwawezesha kuanzisha biashara na kujiajiri. Kwa maana hiyo mfumo huu wa vikundi na mafunzo ni moja ya njia nyingi za kuwajenga vijana katika kujiajiri na hivyo kupunguza tatizo la ajira kwa vijana.

***Wanavikundi***

Nina imani kuwa  nidhamu na uadilifu ndio msingi wa mafanikio ya vikundi vyenu. Kwani katika vikundi vinavyohusisha fedha hususan mikopo ni rahisi sana kushindwa ikiwa hakuna uadilifu.

Kwa kuwa ninyi mmefanikiwa, nawashauri sasa muangalie uwezekano wa kukua zaidi kwa kuanzisha Taasisi yenu ambayo itakuwa na uwezo wa kuwakopesha fedha nyingi zaidi na hivyo kupanua biashara zenu. Lakini pia mjipange kutumia taasisi za fedha zilizopo kwa ajili ya kupata elimu ya fedha zaidi ili muweze kupata mikopo ya kufanya biashara kubwa zaidi.

Nitumie fursa hii kuwaomba wadau mliopo, kuwaunga mkono wanavikundi hawa kwa kuonesha fursa zilizopo ili waweze kuzitumia kwa ajili ya kujiendeleza kiuchumi. Lakini pia wapo watoa huduma za jamii kama Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya NHIF, Mfuko wa hifadhi ya jamii GEPF, Benki ya Wanawake ambao wanazo fursa nyingi kwa ajili ya wanavikundi ambao wako katika sekta hii isiyo rasmi ya ajiri ambao nao wanahitaji huduma zenu, tafadhali wafuateni na muwaelimishe.

***Mabibi na Mabwana,***

Nimalizie kwa kuwatakia kila la kheri na fanaka wanavikundi wote katika kutekeleza mipango yenu ya kujikwamua kiuchumi, Mwenyezi Mungu awasimamie ili muweze kufanikisha hayo.

Baada ya kusema hayo, sasa nazindua rasmi UMOJA WA VIKUNDI VYA WAMA WILAYA YA KINONDONI - (UWAMAKI ) LEO TAREHE 18 DISEMBA,2014.

***MUNGU IBARIKI TANZANIA! MUNGU IBARIKI AFRIKA***

***ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA!***